

We Care - Therapy Grant Guidelines (Tunajali - Miongozo ya Ruzuku ya Tiba)

Kwa watoto walio na utambuzi (diagnosis) au hali ya ugonjwa inayohitaji tiba inayoendelea. Hutoa \$2000 ili kusaidia kulipia gharama ya matibabu au tathmini inayofanywa na mtaalamu anayestahiki katika kipindi cha miezi 12.

Tiba zinazostahiki ni:

- Tiba ya fiziolojia (Physiotherapy)
- Tiba ya Matumizi ya Viungo vya Mwili (Occupational Therapy)
- Tiba ya Kuzungumza (Speech Therapy)
- Tiba ndani ya maji (Hydrotherapy)
- Saikolojia
- Zoezi la Fiziolojia (Exercise Physiology)

Kustahiki

- Watoto wa umri wa miaka 0 - 18
- Wakazi wote wa NSW na ACT wanaweza kutuma maombi, ikijumuisha wasio raia na wenye viza ya muda /wakimbizi.
- Utambuzi rasmi uliothibitishwa na daktari wa watoto, daktari wa akili, au mtaalamu wa afya shirikishi.
AU
- kushukiwa kuwa na hali ambayo huenda ikahitaji matibabu endelevu lakini bado haijatanguliwa rasmi
- Haistahiki kwa NDIS (Mpango wa Kitaifa wa Bima ya Walemavu)
AU
- yamekubaliwa kwenye NDIS, na yana hali zenye kuzidisha ambazo zinahitaji usaidizi wa kifedha kwa ajili ya matibabu wakati wa kusubiri mpango wa NDIS.
- jumla ya mapato ya jumla ya familia ni chini ya \$80,000 kwa mwaka (ikijumuisha usaidizi wa watoto, mapato ya uwekezaji, mapato ya ng'ambo au mapato mengine yoyote)

Maombi

- Maombi yanatarajiwa kuwa ya ukweli na yenye kutegemea mambo ya ukweli, sehemu zote zimejazwa kamili na hati (documents) zilizoombwa ziambatishwe
- Hutengenezwa kwa niaba ya mtoto na mzazi/mlezi au mtu wa usaidizi aliyetambuliwa zaidi ya miaka 18
- *Tafadhali kumbuka kuwa fomu ya maombi iko mtandaoni na iko kwa Kiingereza. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kusoma na kuandika kwa Kiingereza, tafadhali tafuta usaidizi kutoka kwa mtu wa usaidizi kama vile ; mtaalamu wa matibabu, mfanyakazi wa kesi, mwalimu, mtoa tiba, mwanafamilia au rafiki.*

Nyaraka (documents) zinazohitajika

Viambatisho vifuatavyo lazima vijumuishwe kwenye ombi

1. **Barua iliyotiwa saini na GP au Daktari wa watoto** kwenye karatasi yenye kuwa na kichwa cha maelezo ya hospitali au kliniki inayoonyesha:

- utambuzi/hali ya mtoto
- rufaa kwa tiba iliyoombwa

Hati (document) iliyoandikwa ndani ya miezi mitatu ya maombi

2. **Mapato ya Kaya (familia)** - Kwa kila mzazi/mlezi ambaye anawajibika kifedha kwa mtoto moja ya yafuatayo lazima iwasilishwe:
 - Ikiwa unapokea Malipo ya Centrelink - toa Taarifa yako ya Mapato ya Centrelink ya hivi majuzi
 - Ikiwa mzazi/mlezi ameajiriwa - toa hati 2 za malipo (payslips) za hivi majuzi zinazoonyesha mapato ya kila mwaka
 - Ikiwa mzazi/mlezi hapokei Malipo ya Centrelink na hajaajiriwa - toa taarifa za benki kwa miezi 3 iliyopita.
 - Ikiwa mzazi ameajiriwa - toa taarifa za benki za miezi mitatu iliyopita.
3. **NDIS** - Ikiwa umetuma maombi ya NDIS, tafadhali pakia (upload) mawasiliano yako ya hivi majuzi.

Maombi yasiyostahiki

- Ombi la kufadhili gharama ya uchunguzi na daktari wa watoto au mtaalamu mwingine wa matibabu
- Ombi la matibabu halijaorodheshwa kama linalostahiki katika miongozo hii
- Ufadhili wa kurudi nyuma - huduma zinazotolewa tu baada ya idhini (approval) ya ruzuku ndizo zinazostahiki
- Mwombaji ametuma maombi ya Ruzuku ya We Care Therapy Grant ndani ya miezi 12 iliyopita

Uidhinishaji (approval) wa maombi ya ruzuku

Maombi yanaidhinishwa na Variety's Grants Committee (Kamati ya Ruzuku ya Variety). Arifa kupitia barua pepe inaweza kuchukua hadi wiki 8.

Maombi ambayo hayajafanikiwa

- Maombi ambayo hayajafanikiwa yanatokana na uamuzi wa Kamati ya Ruzuku na inastahili kutuma maombi upya baada ya miezi 12.

Maombi ambayo yamefanikiwa

- Barua ya matokeo inatumwa kupitia barua pepe inayoonyesha jinsi ya kutumia ruzuku.
- Ruzuku inaisha muda miezi 12 baada ya tarehe kwenye barua ya matokeo

Malipo ya Huduma za Tiba

- Mtoa huduma wa matibabu lazima atoe ankara ya kodi (tax invoice) itakayolipwa kwa Variety kwa bidhaa iliyoidhinishwa
- Variety NSW/ACT haitoi pesa moja kwa moja kwa waombaji
- Ni wajibu wa mzazi/mlezi kupakia (upload) ankara za kodi (tax invoice) kwenye lango la mtandao la Variety (online Variety portal) kwa malipo kama ilivyoelekezwa katika barua ya matokeo.
- Fedha zozote ambazo hazijatumika zitapotezwa baada ya tarehe ya kumalizika muda wa ruzuku

Taarifa zaidi

Ikiwa unahitaji maelezo zaidi, tafadhali usisite kuwasiliana na timu ya Usaidizi kwa Watoto kwenye kidssupport@variety NSW.org.au